# MFUKO WA UDHAMINI WANAWAKE TANZANIA(WFT TRUST)

# WITO WA MAOMBI YA KUTEKELEZA MIRADI KUENDELEZA HAKI ZA WANAWAKE, WASICHANA NA WATOTO TANZANIA KWA MWAKA 2026.

The Registered Trustees of Women Fund Tanzania (WFT Trust) ni Mfuko wa kwanza wa uwezeshaji wa kutetea haki za wanawake ulioanzishwa kwa ajili ya wanawake, wasichana, na watoto. Mfuko huu una malengo mahsusi ya kuona jamii yenye usawa na haki kwa kuondoa visababishi vinavyopelekea mgawanyo usio sawa wa mamlaka, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa usawa wa kijinsia, na mifumo mingine kandamizi pamoja na mitazamo hasi ya kijamii katika nyanja mbalimbali. WFT Trust inafanya hivi kwa kutoa ruzuku kwa mashirika yanayofanya utetezi na uchechemuzi wa haki za wanawake, wasichana, na watoto pamoja na kuwezesha ujenzi wa TAPO la wanawake la kifeminia ili kuleta nguvu na sauti za pamoja ili kuleta mabadiliko endelevu ya haki za wanawake na watoto na kwa jamii nzima.

WFT-T, kwa kushirikiana na Msichana Initiative na Cuso International, na kwa ufadhili wa Global Affairs Canada, inatekeleza mradi wa miaka mitano unaoitwa **Renewed Women's Voices and Leadership Project (RWVL–T).** Mradi huu unalenga kuimarisha na kuwezesha mashirika ya utetezi wa haki za wanawake, (WROs) pamoja na mashirika yanayoongozwa na wafeminia vijana wa kike (YFOs) yanayofanya kazi ya kutetea na kulinda haki za wanawake na wasichana.

Awamu ya kwanza ya Programu ya WVL ilitekelezwa kuanzia mwaka 2019 hadi 2024, ikiwa na lengo kuu la kuimarisha uwezo wa taasisi za wanawake,ujenzi wa TAPO lenye nguvu na kuendeleza utetezi wa sera, ili kupaza sauti ya wanawake na wasichana katika nyanja mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisera.

Kwa sasa, kupitia Mradi wa Renewed Women's Voices and Leadership Project (RWVL–T) (2025–2030), juhudi zinaelekezwa katika kufanikisha matokeo makuu yafuatayo ya kimkakati:

- Kuimarishwa kwa uendelevu wa taasisi za mashirika ya ndani ya haki za wanawake (WROs) na mashirika yanayoongozwa na wanafeminia vijana (YFOs), ili yaweze kutekeleza kikamilifu na kwa ufanisi majukumu yao ya kuendeleza usawa wa kijinsia (Gender Equality – GE).
- Kuimarishwa kwa ubora na ushawishi wa programu pamoja na utetezi unaofanywa na WROs na YFOs, kwa lengo la kuendeleza usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake na wasichana kushiriki kikamilifu katika nyanja za kijamii, kiuchumi na kisiasa.
- Kuongezeka kwa ufanisi na mshikamano wa majukwaa, mitandao na miungano ya haki za wanawake katika ngazi za kitaifa, kikanda na kimataifa, ili kuleta mabadiliko chanya ya sera, sheria na mitazamo ya kijamii yanayochochea haki na usawa kwa wanawake na wasichana.

**Nani anaweza kutuma maombi**

WFT Trust kwa kushirikiana na Msichana Initiative Organization (MIO) wanapokea maombi kutoka kwa mashirika ya haki za wanawake, mashirika yanayoongozwa na wanaharakati vijana wa kike, pamoja na mashirika ya kijamii (Community Based Organizations – CBOs) yanayofanya kazi za utetezi,uchechemuzi na ulinzi wa haki za wanawake na wasichana.

Maombi yanakaribishwa kutoka kwa mashirika yaliyoanzishwa na yanayofanya kazi ndani ya Tanzania. Tafadhali pitia tovuti zetu: **https://wftrust.or.tz** na **https://msichana.or.tz**

**Maeneo muhimu ya ufadhili katika 2026 ni:**

1. **Kuimarisha Ushiriki wa Wanawake na Wanaharakati Vijana wa Kifeminia katika Uongozi na Maamuzi** – kushughulikia changamoto zilizopo na zinazoibuka ambazo zinazuia wanawake na wanaharakati vijana wa kifeminia kushiriki kikamilifu katika mifumo ya uongozi na mchakato wa kufanya maamuzi. Hii inahusisha kuhoji na kubadili mifumo na miundo kandamizi, mila na desturi, mitazamo hasi ya kijamii, pamoja na nguvu za kimamlaka (power dynamics) zinazowazuia wanawake na wanaharakati vijana wa kifeminia kuchukua na kushika nafasi za uongozi katika ngazi za maamuzi ndani ya jamii zao, taasisi za kibiashara (sekta binafsi), na katika maeneo mengine ya huduma za umma.
2. **Ushiriki wa Kisiasa na Uongozi wa Wanawake** – kwa kuzingatia hasa kushughulikia rushwa ya ngono (sexual corruption/sextortion), mauaji ya wanawake na wasichana kwa misingi ya kijinsia (femicide), ukatili wa kijinsia mtandaoni (unyanyasaji wa mtandaoni/ cyberbullying), pamoja na aina za ukatili unaohusiana na afya ya akili unaowaathiri wanawake, wasichana na wanaharakati vijana wa kifeminia, hususan wale wanaokumbwa na mifumo kandamizi ya kitamaduni na mijadala yenye madhara katika jamii za vijijini na mijini.

Eneo hili pia linajumuisha haki na usawa katika elimu, kwa kuvunja na kubadilisha mifumo ya kitamaduni na kitaasisi inayodumisha ukosefu wa usawa na kuwazuia wanawake, wasichana na wanaharakati vijana wa kifeminia kushiriki kikamilifu na kwa usawa katika elimu. Hii ni pamoja na kukabiliana na utamaduni wa ubakaji (rape culture), mimba za utotoni, ndoa za utotoni, na kuendeleza juhudi za kuwawezesha wasichana kurejea na kuendelea na masomo katika mfumo rasmi wa elimu.

3. **Ujenzi na Uimarishaji wa Harakati (Movement Building and Strengthening)** – Afua na mikakati inayochochea ukuaji, upanuzi na kuimarika kwa harakati zinazojikita katika misingi ya kifeminia, kwa kuzingatia mbinu jumuishi zinazotambua mchangamano wa utambulisho na uzoefu (intersectional), kuunganisha vizazi mbalimbali (intergenerational), na kuhakikisha ushirikishwaji wa makundi yote.

Lengo ni kuharakisha mabadiliko ya kimfumo na ya mageuzi yanayozingatia misingi ya kifeminia ndani ya harakati za wanawake, wanaharakati vijana wa kifeminia na watoto, pamoja na kuimarisha ushirikiano kati ya harakati hizi na harakati nyingine za kijamii. Hii ni pamoja na harakati zinazotetea haki za watu wenye ulemavu, haki za mtoto, haki za afya ya uzazi na jinsia, na haki ya mazingira, kwa ajili ya kujenga mshikamano wa pamoja na nguvu ya pamoja katika kuleta mabadiliko endelevu na ya haki katika jamii.

4. **Haki ya Kiuchumi na Uendelevu** – kuvunja na kubadilisha vikwazo vya kisera na kitamaduni vinavyopunguza au kuzuia ushiriki kamili na wenye tija wa wanawake, wasichana na wanaharakati vijana wa kifeminia katika shughuli za kiuchumi, na vinavyowakosesha fursa ya kunufaika na sekta pana za uchumi kama vile mafuta, gesi na rasilimali za madini (extractives).

Eneo hili pia linahusisha ushiriki katika mikakati ya kisera ya ngazi mbalimbali inayolenga kukuza sauti, uwakilishi na ushiriki wa wanawake, wasichana na wanaharakati vijana wa kifeminia katika mipango ya upangaji wa bajeti unaozingatia usawa wa kijinsia (gender budgeting), pamoja na kuimarisha upatikanaji wa huduma za ujumuishaji wa kifedha katika sekta mbalimbali za maendeleo.

5. **Haki ya Mazingira na Jinsia** – kushughulikia changamoto za kisera, kisheria na kitamaduni zinazowazuia wanawake na wasichana katika kutumia sauti zao na mamlaka yao ya kujiamulia (agency). Hii inahusisha pia kukabiliana na athari hasi za uharibifu wa mazingira, kwa kuzingatia kwa umakini masuala ya mabadiliko ya tabianchi na haki za umiliki na matumizi ya ardhi kwa wanawake, wasichana na wanaharakati vijana wa kifeminia kote Tanzania.
6. **Kukuza na Kulinda Haki za Afya ya Uzazi** – Maombi yanakaribishwa kwa ajili ya afua zinazokuza mbinu zinazozingatia haki za binadamu na misingi ya kifeminia katika kushughulikia haki za afya ya uzazi. Hii inajumuisha pia kuimarisha na kujenga harakati za kijamii zitakazoongeza uwezo wa wadau muhimu kutetea na kushughulikia masuala yanayowanyima wanawake, wasichana balehe na wanaharakati vijana wa kifeminia upatikanaji wa taarifa sahihi, stahiki na zinazozingatia jinsia kuhusu afya ya uzazi.

Afua hizi zinapaswa kujumuisha, lakini si kwa ukomo, upatikanaji wa huduma bora za afya ya uzazi, haki ya kufanya maamuzi yenye taarifa sahihi (informed decision-making), kuimarisha uwezo wa kujiamulia (agency), na kushiriki kikamilifu katika masuala yanayowahusu. Aidha, zinatarajiwa kuweka mikakati madhubuti ya kuongeza upatikanaji wa huduma na taarifa kwa makundi yaliyo pembezoni, ikiwemo watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyo katika mazingira ya hatarishi.

7. **Masuala ya Haki ya Afya ya Uzazi** - Maombi yako wazi kwa ajili ya kutekeleza shughuli zinazolenga kukuza uelewa wa haki pamoja na masuala mtambuka ya afya ya uzazi kwa wanawake na hatua za kusaidia harakati za utetezi unaojikita katika kushughulikia maswala yanayowanyima wanawake na wasichana kufanya maamuzi ya msingi na yanazozingatia ufeminia na kushughulikia haki ya uzazi kwa ajili ya ujenzi wa harakati za kijamii zinazoboresha uwezo wa wahusika wakuu kutetea na kurahisisha upatikanaji wa taarifa muhimu za haki ya afya ya Uzazi, ikiwa ni pamoja na huduma, kufanya maamuzi sahihi, ushiriki na kuwawezesha kutekeleza mikakati ya kuimarisha upatikanaji wa haki za afya ya uzazi kwa makundi yaliyo pembezoni ikiwa ni pamoja na walemavu na makundi mengine.

8. **Kujenga vuguvugu la kiharakati la kuleta pamoja wanawake na wasichana kimkakati na kuimarisha TAPO la wanawake Tanzania** - Kutekeleza shughuli mbalimbali za kukuza njia za makutano katika kuharakisha mabadiliko ya ndani ya harakati za wanawake na harakati zingine za kijamii pamoja na zile zinazofanya kazi kuendeleza haki za walemavu, haki za watoto, haki za afya ya uzazi, haki za wahamiaji na haki ya mazingira kwa hatua za pamoja na utekelezaji wa pamoja. Kuimarisha harakati za kubadilisha mifumo, sera, na mitizamo ya kijinsia katika tamaduni, kanuni za kijamii, na pia katika mifumo ya sera na sheria katika viwango tofauti.

**Madirisha kwa Ajili ya Maombi ya Ufadhili:**

**1. DIRISHA LA KIWANGO CHA KATI**

Miradi chini ya Dirisha hili inapaswa kuzingatia afua zinazolenga kusaidia mashirika ya haki za wanawake, wasichana na watoto kujenga na kuimarisha uwezo wao wa kimawazo (conceptual capacities) na kiutendaji/ kitaasisi, pamoja na kuendeleza utaalamu wa kujenga mitandao na kushirikiana maarifa ndani ya harakati za wanawake na wasichana.

- Muda wa ruzuku unapaswa kuwa kati ya miezi 6 hadi mwaka 1
- Miradi lazima ilenge kutoa sauti na kuongeza utambulisho/uonekano wa wanawake, wanaharakati vijana wafeminia na wasichana katika masuala kadhaa kama yalivyoainishwa katika wito wa kuwasilisha mapendekezo ya miradi (Call for Proposals)
- Dirisha hili liko wazi kwa taasisi zinazoongozwa na

wanawake na wanaharakati vijana wafeminia katika ngazi za mitaa/wilaya/mikoa na kitaifa, zinazohitaji rasilimali za kifedha kwa ajili ya kuimarisha uwezo wa taasisi zao, iwe kwa kuendeleza au kupanua mradi uliopo, au kwa kuanzisha mradi mpya unaoshughulikia maeneo ya kimkakati yaliyoainishwa katika wito wa mapendekezo, pamoja na kuimarisha miungano ya kimkakati na mitandao ndani ya harakati za wanawake na wanaharakati vijana wafeminia katika ngazi mbalimbali.

**3. DIRISHA LA KIMKAKATI**
Dirisha la Kimkakati (Strategic Window) linalenga kufadhili miradi au afua za muda mrefu zenye kipindi cha hadi miaka 2, pamoja na shughuli zinazolenga kujenga na kuimarisha harakati, majukwaa au miungano ya kifeminia. Dirisha hili pia linaweza kutumika kusaidia mashirika ya haki za wanawake (WROs) na mashirika yanayoongozwa na wanaharakati vijana wafeminia (YFOs) yanayokua na yanayohitaji ufadhili wa msingi (core funding) kwa ajili ya kuimarisha uwezo wa kitaasisi na kiutendaji.

Kwa namna ya kipekee, wanufaika wanaohitimu kutoka Dirisha la Kati (Middle Window) pamoja na mashirika ya kitaifa ya haki za wanawake yaani mashirika ya kitaifa ya wanawake na wanaharakati vijana wa wafeministi yenye uwezo wa kujenga harakati kupitia upanuzi wa wigo wa ushiriki (reach), uundaji wa ajenda (agenda setting), na ujenzi wa msingi wa wanachama au wadau (constituent base-building interventions) yanafaa zaidi kwa dirisha hili kutokana na ukuaji wao na wajibu wao katika kazi za kujenga harakati au miungano/majukwaa.

Dirisha hili pia inaweza kuombwa kwa ajili ya kusaidia kazi za ushirikiano (cross-movement work) kati ya harakati mbalimbali za wanawake, wafeminia vijana, wasichana na watoto. Mashirika ya kifeminia ya haki za wanawake yenye uwezo madhubuti wa kitaasisi, utaalamu, mitandao na uelewa wa muktadha wa ndani, ili kushirikiana na wadau wengine wa ngazi za mitaa na kitaifa katika kuimarisha mikakati ya ujenzi wa harakati za wanawake katika sekta mbalimbali, yanahimizwa kuwasilisha maombi.

Katika muktadha huu, tunapokea mapendekezo yanayolenga kuanzisha na kupanua afua zinazochochea utetezi wa pamoja (collective/joint advocacy actions), kuunda majukwaa yafanyayo kazi pamoja (cross-border platforms), kuimarisha mitandao ya pamoja, na kukuza ujifunzaji wa pamoja ndani ya sekta mbalimbali za harakati za wanawake, wafeminia vijana, wasichana na watoto nchini.

**TUNATAFUTA NINI?**
Waombaji wanapaswa kuhakikisha andiko lao la mradi yanafuata muongozo kama ilivyoainishwa hapa chini:

**I. KUOANA KWA MALENGO YA MRADI NA MAHITAJI MAKUU YA KIJINSIA KATIKA JAMII**

- Washirika wanaoshiriki azma yetu ya kuchangia kuondoa ukosefu wa usawa wa kijinsia, mila na desturi za kibaguzi, pamoja na mifumo kandamizi, kupitia kuimarisha uwezo wa taasisi na kujenga harakati za wanawake na wanaharakati vijana wa kifeminia. Aidha, kazi zao zinapaswa kuendana na maeneo ya kimkakati (thematic areas) tuliyoyabainisha.

**II. UWEZO WA MTANDAO, SHIRIKA/KIKUNDI & UFAHAMU WA TATIZO LA MSINGI LA KUTATULIWA NA MRADI**

- Andiko la mradi linapaswa kuhakikisha uhusiano thabiti kati ya tatizo la kushughulikiwa na mikakati na matokeo yanayoweza kupimika yanayotarajiwa kupatikana kutokana na utekelezaji wa mradi
- Andiko la mradi linapaswa kuakisi ushiriki wa washikadau mbalimbali (ndani ya mtandao wa wanawake, wafeminia vijana na katika mitandao mingine) hasa katika utekelezaji wa kuunda/kuimarisha mitandao ya utendaji kazi, mitandao na majukwaa (hasa kwa madirisha 2&3)
- Andiko la mradi linapaswa kuonesha dhamira ya uendelevu, uvumbuzi, ubunifu.
- Maandiko hayo ya mradi yanapaswa kujumuisha shughuli zitakapopangwa kufanyika katika siku za maadhimisho ya kikanda na kimataifa kama vile Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike, Siku ya Kimataifa ya Wanawake wa Vijijini na Siku 16 za Uanaharakati za Kupinga Ukatili wa Kijinsia.

**Namna ya kutuma Maombi**
Tafadhali tembelea tovuti ya WFT Trust (https://wftrust.or.tz) pamoja na tovuti ya Msichana Initiative (https://msichana.or.tz) ili kutuma maombi ya ruzuku

**Maombi ya Ruzuku hizi yatafuata utaratibu huu:**
Maombi yote yanapaswa kuwasilishwa **mtandaoni kupitia sehemu ya Grants katika tovuti ya Women Fund Tanzania Trust.** Waombaji wanatakiwa kubofya kitufe cha "Apply" kilichopo chini ya sehemu ya Grants na kujaza fomu ya maombi ya mtandaoni kulingana na maelekezo yaliyotolewa.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali piga simu: +255 753 912 130

**Tafadhali kumbuka:**
Hakuna ofa, malipo, zawadi, uzingatiaji au manufaa ya aina yoyote, ambayo yanajumuisha au yanaweza kufasiliwa kuwa ni kitendo haramu au ulaghai, yatatolewa, moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja, kama kichocheo au zawadi kwa ajili ya mafanikio ya ombi.

Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha maombi itakuwa Ijumaa, Aprili 6, 2026 saa kumi alasiri.

Waombaji wote waliofanikiwa na wasiofanikiwa katika maombi yao watajulishwa ifikapoa tarehe 31 Juni 2026